



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA KIGAMBONI



[Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa Kigamboni]

Simu: +255 22-2928468
Fax: +255 22-2928469
Baruapepe: info@kigambonimc.go.tz
Tovuti: www.kigamboni.go.tz

S.L.P. 36009,
KIGAMBONI,
DAR ES SALAAM,
TANZANIA.

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. AC.23/113/02

Tarehe: 18/3/2024

TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA YA MKATABA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni anawatangazia Wananchi wote raia wa Tanzania wenye sifa kuomba nafasi za kazi zilizo rodheshwa hapo chini.

1. MTEKNOLOJIA MIONZI DARAJA II- (NAFASI 4)

a) Sifa za mwombaji:-

Kuajiriwa wenye Stashahada katika fani ya Uteknolojia wa mionzi (radiolojia) kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Mabaraza pale inapohusika

b) Majukumu ya kazi:

- (i) Kuwapima wagonjwa wanaolekezwa kwenye eneo lake la kazi
- (ii) Kutunza mitambo na vifaa vya Radiolojia katika eneo lake la kazi
- (iii) Kukagua picha za X-Ray zilizopimwa kwa ubora na kutosheleza (diagnostic quality)
- (iv) Kutunza picha za wagonjwa hadi majibu yanapowafikia madaktari waliowatuma wagonjwa
- (v) Kusimamia watumishi walio chini yake
- (vi) Kutoa Ushauri kuhusu masuala ya na kazi za Radiolojia na Mionzi katika eneo lake la kazi.
- (vii) Kuandaa vifaa vya tiba/uchunguzi na kusimamia utakasaji vifaa katika eneo lake la kazi (sterilization)
- (viii) Kutoa mafunzo ya awali kwa watumishi wanaopangiwa kazi katika eneo lake la kazi.
- (ix) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

MSANIFU MAJENGO DARAJA LA II (NAFASI 1)

a) Sifa za mwombaji:-

Kuajiriwa wenye Shahada/Stashahada ya juu ya Uhandisi katika Vyuo Vikuu vinavyotambuliwa na Serikali katika mojawapo ya fani za Uhandisi

b) Majukumu ya kazi:

- i. Kufanya kazi chini ya uangalizi wa msanifu majengo aliyesajiliwa na Bodi ya Usajili husika kama " Professional Archtect" ili kupata uzoefu unaotakiwa
- ii. Kufanya kazi kwa vitendo katika fani zinazomuhusu ili kumuwezesha kupata sifa za kutosha kusajiliwa na Bodi ya Usajili inayowahusu Wasanifu majengo
- iii. Kufuatilia upatikanaji wa taarifa na taaluma za Usanifu wa Majengo
- iv. Kupitia mapendekezo ya miradi (project proposals) mbalimbali ya majengo yanayowasilishwa Wizarani

MKADIRIAJI UJENZI DARAJA LA II (NAFASI 2)

a) Sifa za mwombaji:-

Kuajiriwa wenye Shahada/Stashahada ya juu ya Uhandisi katika Vyuo Vikuu vinavyotambuliwa na Serikali katika mojawapo ya fani za Uhandisi

b) Majukumu ya kazi:

- i. Kufanya kazi chini ya uangalizi wa msanifu majengo aliyesajiliwa na Bodi ya Usajili husika kama " Professional Quantity Surveyor" ili kupata uzoefu unaotakiwa
- ii. Kufanya kazi kwa vitendo katika fani zinazomuhusu ili kumuwezesha Mkadiriaji Ujenzi kupata sifa za kutosha kusajiliwa na Bodi ya Usajili inayomuhusu
- iii. Kukusanya taarifa na takwimu kuhusu miradi mbalimbali kuhusu bei za vifaa vya Majengo ndani na nje ya nchi
- iv. Kupitia mapendekezo ya miradi (project proposals) mbalimbali ya Majengo yanayowasilishwa Wizarani na kutoa ushauri unaotakiwa

2. MASHARTI KWA UJUMLA:


- (i) Mwombaji awe raia wa Tanzania.
- (ii) Mwombaji awe na Umri usiopungua miaka 18 na awe hajawahi kupatikana na kosa lolote la jinai, kufungwa jela na kufukuzwa kazi katika Utumishi wa Umma.
- (iii) Waombaji waambatishe maelezo yao binafsi (CV).
- (iv) Maombi yote yaambatane na nakala ya vyeti vya taaluma, vyeti vya kidato cha nne IV au VI, cheti cha kuzaliwa na picha mbili za rangi za hivi karibuni na ziandikwe majina nyuma.

- (v) *Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa nakufanyiwa ulinganishi na Mamlaka husika TCU, NACTE na NECTA na taarifa ya uhakiki iambatishwe kwenye maombi.
- (vi) Testimonials, provisional results, Statement of Results hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita (FORM IV and FORM VI RESULT SLIPS) HAVITAKUBALIWA.
- (vii) Uwasilishwaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria
- (viii) Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **.31 Machi, 2024. Saa 9.30** alasiri.

Maombi yatumwe kwa Anuani ifuatayo:-

**Mkurugenzi wa Manispaa,
Halmashauri ya Manispaa Kigamboni,
S.L.P. 36009,
KIGAMBONI - DAR ES SALAAM.**

Limetolewa na:-



E. N. Kiwale

MKURUGENZI WA MANISPAA YA KIGAMBONI.

**MKURUGENZI WA MANISPAA
KIGAMBONI**

Nakala: Tovuti ya Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni.

Mbao za Matangazo